



# **BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

## **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

### **BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI**

#### **MKUTANO WA PILI**

#### **Kikao cha Tisa – Tarehe 1 Juni, 2016.**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua zitasomwa.

#### **I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

##### **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2016/2017.

##### **Mwenyekiti Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala:**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2016/2017.

##### **Mwenyekiti Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC):**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) kuhusu Hotuba ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) kwa Mwaka 2016/2017.

**II. MASWALI:****WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA:**

44. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) lilizindua huduma ya kununua umeme kwa kutumia simu za mkononi kupitia Kampuni ya Zantel ambazo zimeyeyuka kama barafu katika jua na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar.

- a) Utaratibu wa watu kununua umeme kwa kupanga foleni katika vituo inapelekea Shirika kupiga hatua ya Maendeleo au kurudi nyuma.
- b) Kwa kuwa wananchi wanaendelea kuteseka kwa muda mrefu kwa kutoweka huduma hiyo kwanini Shirika limekaa kimya kueleza wananchi sababu za kutoweka kwa huduma hiyo wakati wananchi hufaidika na huduma hiyo.
- c) Kwa kuwa wananchi wamekuwa wakikaa muda mrefu kwenye vituo wakati muda huo ni wa harakati za kiuchumi, kwanini Shirika la Umeme hawatafuti Kampuni nyengine za simu na kuingia Mkataba wa kuuza umeme zaidi ya Kampuni moja kama ilivyo kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI:**

59. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Chukwani) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kumekuwa na tatizo la muda mrefu la matumizi mabaya ya barabara ya kuanzia mzunguko wa mazizini mpaka fumba ambapo waendesha vyombo vya usafiri vya moto kama gari, vespa na pikipiki huendesha kwa mwendo wa kasi kupita kiasi na kusababisha ajali na upotevu wa maisha na ulemavu hasa maeneo ya skuli.

- a) Je lini barabara ile itawekwa matuta ili kudhibiti madereva wa sasa hasa vijana wanao kimbizana na vespa (t-one).
- b) Kutowekwa matuta barabarani hamuoni kwamba inazidisha ongezeko la ajali za kizembe ambazo waathirika wakubwa ni wanafunzi wa skuli ilimopita barabara hiyo.

**WIZARA YA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

81. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Mchezo wa Mpira wa Miguu (Football) ni miongoni mwa mchezo mkubwa unaopendwa na watu wengi hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Hali hii imechangiwa na jamii yenyewe kuweka nguvu kubwa katika kuukuza, kuushabikia na kuutangaza mchezo huu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha michezo mengine kama vile, kuvuta Kamba, kufukuza kuku, karata, bao nk.

**WIZARA YA AFYA:**

18. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) -  
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga mji mpya wa Tunguu, lakini kumekuwa na tatizo la huduma za afya, kwa kuzingatia kuwa kuna Tunguu Dispensary pekee inayotumiwa na watu wa Binguni, Tunguu, Jumbi na Bungi.

Je, Wizara haioni umuhimu wa kujenga dispensary nyengine kwa wananchi wa Bungi kwa sababu wapo wananchi wengi.

**III. HOJA ZA SERIKALI:****Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:**

Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka 2016/2017.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:**

Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2016/2017.

Zanzibar,  
1 Juni, 2016.

(Raya Issa Msellem)  
**KATIBU WA BARAZA**